**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**

**SHULE YA SEKONDARI MINAKI.**

S.L.P. 28004,
**KISARAWE.**

**WEBSITE**: **www.minakischool.ac.tz**
**MOB**: MKUU WA SHULE - 0717 505 951
MAKAMU M/SHULE - 0692 471345
MWL. WA MALEZI - 0752 005 937

**Kumb. Na. MSS.210/185**

**Kwa ………………………………………….**
**...……………………………………..**

**YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MINAKI – 2022/ 2023.**

Nafurahi kukujulisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha tano mwaka 2022/2023. Napenda kuchukuwa nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha hapa shuleni na bila shaka utapenda kuishi na kunufaika na mambo yanayoendeshwa hapa shuleni. Nategemea kwamba muda wote utakapokuwa katika shule hii utashirikiana na wanafunzi wenzako, walimu na wafanyakazi wasio walimu katika kutoa mchango wako wa mawazo na vitendo ili kuleta na kudumisha sifa nzuri na maendeleo ya shule hii.
Shule hii ya Minaki ipo katika Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, umbali wa kilometa 9 kutoka Gongo la mboto- Dar es salaam. Unapokuja Minaki itabidi upande mabasi yanayokwenda Kisarawe. Mabasi yanaanzia safari katika kituo cha Gongo la mboto jijini Dar es Salaam.
Pamoja na barua hii naambatanisha taarifa zifuatazo:

- **(a)** Fomu ya kujiunga na shule (Joining Instructions) – hakikisha unaisoma neno wa neno.
- **(b)** Fomu ya taarifa za mwanafunzi (MSS.K5. A) na fomu ya uthibitisho (MSS.K5. B). Fomu hizi zitatakiwa kujazwa Na mzazi/mlezi na utazileta shuleni na kuzikabidhi siku ya kuripoti.
- **(c)** Fomu ya uchunguzi wa afya (MSS.K5.ME).
- **(d)** Fomu ya sheria za Shule ambayo mzazi/mlezi na wanafunzi wanatakiwa kusaini kuonyesha wamezisoma na kuzielewa ( MSS.K5 .C).

Mwisho, nakufahamisha kuwa muhula wa masomo unaanza tarehe -------------- hivyo, unatakiwa **ufike shuleni** tarehe --------------- kabla **ya saa kumi na mbili (12:00) jioni.** Mara ufikapo shuleni utapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atakupeleka ofisi ya malezi ambapo utasajiliwa. Kama utachelewa kuripoti nitaiarifu Wizara (TAMISEMI) ili waweze kuchagua mwanafunzi mwingine wa kuchukua nafasi yako. Nakutakia safari njema.

Karibu Minaki.

**H. A. Chungu**
**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI MINAKI**

FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)

**Soma maelezo haya kwa uangalifu na umakini na uyatekeleze**;

**1. VIFAA MUHIMU**

**(a)** Unatakiwa uje na **stempu (3)** kwa ajili ya kutuma ripoti ya mitihani kwa Mzazi/**mlezi kuanzia kidato cha tano mpaka utakapomaliza kidato cha sita**.

(b) Mahitaji ya darasani: - kalamu, kasha la vyombo vya hisabati, daftari mbili (2) kwa kila Somo. Daftari zinazotakiwa ni "Quire" 3 au "Quire" 4.

(c) Godoro lenye upana wa futi 2.5

(d) Shuka mbili (rangi ya bluu), blanketi, mto, foronya, taulo na chandarua.

(e) Scientific calculator (Kwa masomo ya science na hisabati.

(f) Shule ina upungufu wa vitabu .Mzazi/mlezi unatakiwa umnunulie mwanao vitabu binafsi angalau kimoja katika moja wapo ya masomo yake.

(g) "Dissecting kit" Kwa somo la Biology.

(h) Kamba rangi ya blue na 'holder' ya kuning'inizia kitambulisho.

**NB:** Orodha ya vitabu Kwa masomo yenye upungufu imeambatanishwa.

**2. SARE**

Unatakiwa uje na sare ya shule kama ifuatavyo na uwe **na idadi ya kutosha** kubadilisha kuanzia mbili nakuendelea. Sababu yoyote ya kutovaa sare haikubaliki;

**a) SHATI;**

Shati rangi nyeupe, mikono mifupi lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto lisilo bana mwili na urefu wa kutosha kuchomekea.

**b) SURUALI;**

- Suruali ya rangi nyeusi (plain black) isiyo na alama yoyote, iwe ya heshima, Marinda mawili kila upande kwa mbele, mifuko ya mbele iwe miwili (mmoja kila upande) na isiwe kama ya suruali ya jeans, isiwe ya kubana /chupa.
- Mfuko wa nyuma mmoja (uwe upande wa kulia na usiwe wa kubandika).
- Pindo za chini za suruali zikunjwe Kwa nje (iwe na "turn up").

**Aidha,** mfano wa kitambaa (sample) cha suruali za shule kinapatikana shuleni.

**c) VIATU**

- Rangi nyeusi vya kufunika mguu.
- Visiwe na soli nene/ soli ya ajabu (kiwe cha heshima)
- Hairuhusiwi kuvaa viatu vya matairi, kandambili au yeboyebo wakati wa masomo darasani na bwaloni /ukumbi wa chakula.

**d) SOKSI**

- Rangi nyeusi isiyo na urembo wowote/rangi nyingine (plain black).
- Ziwe ndefu kiasi cha kukaribia ugoko.

**e) MKANDA** (wa kuvalia suruali)

- Rangi nyeusi na uwe wa ngozi
- Usiwe na madoa au urembo wowote
- Sehemu ya kufungia isiwe na chuma kinene kupita kiasi (uwe wa heshima / usivae mkanda wa begi.

**f) SWETA: -**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sweta hasa ukizingatia kuna msimu wa baridi kali na msimu wa mvua. Kuwa na sweta ni **hiari,** ila ni marufuku kuvaa aina nyingine ya sweta/koti/jaketi tofauti na sare ya shule. Aidha, mfano (sample) wa sweta la shule linapatikana shuleni.

**g) NGUO ZA MICHEZO** Unatakuiwa uje na nguo za michezo ambazo ni bukta, fula ambazo zitavaliwa viwanjani/**muda wa michezo tu**. Aidha, uje na nguo za ndani (boksa, singilendi) saba au zaidi kwa kila nguo. Utaleta bukta na fulana (jezi) kwa rangi ya mchepuo wako kama ifuatavyo: PCM- Blue, PCB –Nyekundu , PGM –Light blue , CBG – Kijani, EGM- Zambarau , HGE – Nyeusi na HKL- Maroon

**h) SARE ZA KUVAA NJE YA MASOMO / "WEEKENDS";**

**(i) Suruali; -**

Suruali za rangi ya 'dark grey' yenye mshono sawa na ile sare ya Shule. Ziwe za kutosha. Nguo zingine hazitaruhusiwa kuvaliwa shuleni hivyo, usilete nguo za nyumbani.
**Aidha,** mfano wa kitambaa (sample) cha suruali hii kinapatikana shuleni.

**(ii) T-shirts: -**

Zitavaliwa nje baada ya muda wa masomo au unapotoka nje ya shule.
Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na Tisheti aina ya Form six rangi ya 'Dark blue' yenye kola.
**Aidha,** mfano (sample) wa Tisheti inayotakiwa inapatikana shuleni.

**NB: -** Mwanafunzi akikamatwa na nguo za nyumbani hatarudishiwa na atapewa adhabu kali.

**3. VYOMBO VYA CHAKULA;**

Nunua vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe pamoja na kijiko. Vyombo vya plastiki haviruhusiwi.

**ANGALIZO;** Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalumu (special diet) kwa wanafunzi Wenye matatizo.

**4. (A)**

| MALIPO SHULENI | KIDATO CHA TANO | KIDATO CHA SITA |
|---|---|---|
| i) Karo (ada) | 70,000/= | 70,000/= |
| ii) Ukarabati wa Samani | 15,000/= | 15,000/= |
| iii) Kitambulisho na Picha | 6,000/= | ---------- |
| iv) Nembo - kwa shati moja | 2,000/= | 2,000/= |
| iv) Tahadhari (caution money) | 5,000/= | 5,000/= |
| v) Taaluma | 20,000/= | 20,000/= |
| vi) Ulinzi/wapishi (VIBARUA) | 30,000/= | 30,000/= |
| vii) Matibabu/Zahanati | 10,000/= | 10,000/= |
| viii) Mitihani ya kijipima | 20,000/= | 20,000/= |
| **JUMLA** | **178,000/=** | **172,000/=** |

**ANGALIZO:** Ada ya Mtihani wa NECTA, MOCK na PRE-NECTA kwa kidato cha sita italipwa kulingana na maelekezo ya viwango vya wakati huo kutoka mamlaka husika.

**(B) UTARATIBU WA KULIPIA;**

Shule haipokei **fedha tasilimu** au hundi kutoka kwa wazazi / walezi wa wanafunzi na badala yake malipo yote yaliyoanishwa kwenye jedwali hapo juu yalipwe kupitia **BENKI** (Isipokuwa fedha zilizoainishwa nje ya jedwali). Malipo yanatakiwa yatumwe shuleni kupitia **Benki ya NMB** (National Microfinance Bank) kwenye tawi lililopo karibu na wewe kabla ya kuja shuleni kwa kufuata utaratibu ufuatao;

- Onana na karani wa Benki na umpe taarifa ya kutaka kutuma ada ya shule. Yeye atakupa maelekezo ya kujaza fomu (Bank Pay in Slip nakala 3).
- Utajaza “Bank Pay in Slip” nakala tatu. Nakala moja itabaki Benki, nyingine kwa mzazi/mlezi na nakala ya tatu utaileta shuleni, na utapewa stakabadhi kwa malipo yote.
- Fedha zote hizi zitumwe kwenye Akaunti ya shule kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| Jina la Akaunti: | **MINAKI SECONDARY SCHOOL** |
| Namba ya Akaunti: | **21401100002** |

**ANGALIZO:** Nakala ya ‘slip’ ya benki utakayoileta shuleni, hakikisha umeiandika kwa nyuma mchanganuo wa fedha uliyoilipa kwa kila mchango.

**5. KARATASI KWA AJILI YA MAZOEZI NA MAJARIBIO: -**

Unatakiwa kuleta karatasi Kwa kila mwaka wa masomo kama ifuatavyo:

1. Photocopy paper (A4 size aina ya ‘double A’ – ukileta aina tofauti haitapokelewa ) ulete ream moja kwa kila mwaka kwa wanafunzi wa HGE, PCM, PCB, na EGM.
2. “Ruled paper” (karatasi za mistari) ulete ream mbili kwa kila mwaka kwa wanafunzi wa CBG, HKL, na PGM.

6. **USAFI:** Unatakiwa kushiriki kazi zote za usafi na utunzaji mazingira kwa kadiri ya Kanuni na taratibu za shule. Hivyo unatakiwa uje na kifaa kimoja cha usafi Kulingana na mchepuo wako wa masomo kama ifuatavyo: -

(a) Fagio refu lenye brashi laini (soft broom) – kwa wanafunzi wa PCM.
(b) Fagio refu lenye mpira wa kukaushia maji (sqeezer) kwa wanafunzi wa EGM.
(c) Fagio la chelewa refu lenye mpini kwa wanafunzi wa HKL.
(d) Fyekeo Kwa mwanafunzi wa PGM.
(e) Hard broom Kwa wanafunzi wa CBG.
(f) Reki Kwa wanafunzi wa PCB
(g) Jembe lenye mpini Kwa wanafunzi wa HGE

7. **MAJI: Shule ina maji ya kutosha,** uje na ndoo mbili za lita kumi kwa ajili ya matumizi yako binafisi kama kufua, kuoga, usafi wa Shule, n.k.

**8. MAWASILIANO: -**

a) Mwanafunzi hatakiwi kuja na simu shuleni, hata hivyo akija nayo aikabidhi ofisi ya Malezi ambapo atarudishiwa anaporudi likizo. Mzazi au mlezi hakikisha mwanao haji na simu shuleni. Iwapo atakamatwa na simu shuleni atanyang’anywa na hatarudishiwa tena. Pia atapewa adhabu kali ikiwemo kutafuta shule nyingine
b) Mawasiliano na mzazi au mlezi yatafanyika kwa utaratibu uliowekwa na shule.

c) Unatakiwa kuripoti ofisi ya malezi kila mara unapotoka likizo kuja shuleni.

**d) FEDHA ZA MATUMIZI: -**

Unashauriwa uje na fedha za kutosha kwa ajili ya : -

(a) Matumizi yako binafsi madogo madogo Kama vile kununua sabuni, dawa ya meno, Kalamu, mafuta ya kupakaa, dawa ya viatu, n.k.

(b) (i) Fedha hizi utakaa nazo mwenyewe. Hata hivyo Kama utakuja na fedha nyingi Itabidi ufungue akaunti ya akiba benki ya NMB (ndiyo iliyo karibu na shule) Kuliko kuweka fedha hizo mfukoni au sandukuni kwani zinaweza kuibwa.

(ii) Utakapohitaji kufungua akaunti, shule itakupa barua ya utambulisho kwa meneja wa benki.

**ANGALIZO:**

1. Shule ya Minaki ni ya bweni hivyo mwanafunzi haruhusiwi kurudi nyumbani au kutoka nje ya shule hadi shule itakapofungwa kwa ajili ya likizo. (ISIPOKUWA KWA KIBALI AU RUHUSA MAALUM). Kama itagundulika umetoka nje ya shule bila kibali / bila kuvaa sare ya shule utapewa adhabu kali .

**2. MZAZI AU MLEZI HURUHUSIWI KUMWONA MWANAFUNZI SHULENI BILA RUHUSA KUTOKA UTAWALA:**

Likitokea hili mwanao atapewa adhabu kali. Siku za kuwaona wanafunzi ni kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 alasiri ili uweze kujua maendeleo ya mwanao kitaaluma na nidhamu yake kwa ujumla.

**3 DHARURA:**

Dharura yoyote itakayompata mwanafunzi kumtaka arudi nyumbani **akiwa katika hali yoyote ile** atakayo kuwa nayo mfano: - ugonjwa, kusimamishwa masomo, n.k. gharama zote zitagharamiwa na mzazi au mlezi. Shule itatoa taarifa tu kwa mzazi / mlezi.

**4 KIKAO CHA WAZAZI / WALEZI NA BODI YA SHULE:**

Kikao cha Bodi ya Shule na wazazi au walezi wote wa wanafunzi pamoja na walimu, kitafanyika tarehe 15-10-2022. Hivyo, wazazi / walezi mnaombwa kujiandaa mapema ili kuweza kuhudhuria kikao hicho (bila kukosa) kitakacho jadili maendeleo ya shule kwa ujumla kwa lengo la kuboresha Taaluma ya shule na ya mwanafunzi mmoja mmoja.

# ORODHA YA VITABU

| IDARA | JINA LA KITABU | MWANDISHI |
|---|---|---|
| | | |
| **HISTORY** | HISTORY OF AFRICA | KELVIN SHILING TON |
| | MASTERING MODERN WORLD AFRICA | NORMAN LOWELL |
| | GENERAL HISTORY OF AFRICA | ADUBOHEN |
| | CONTEMPORY EUROPE SINCE 1870-1958 | KRALTTON |
| | AFRICA THE HISTORY CONTINENT | L.E SMELLGO |
| | GENERAL HISTORY OF AFRICA | MICHAEL TIDDY |
| | ESSENTIALS IN ADVANCED LEVEL HISTORY | SALEH YASSIN |
| **ADVANCED MATHS** | HEINEMANN MODULAR MATHS FOR EDEEXCEL AS AND A-LEVEL PURE MATHS 1 | GEOFF M, M KENWOOD |
| | HEINEMANN MODULAR MATHS FOR EDEEXCEL AS & A-LEVEL PURE MATHS -2 | GEOFF M, M KENWOOD |
| | HEINEMANN MODULAR MATHS FOR EDEEXCEL AS & A-LEVEL PURE MATHS -3 | GEOFF M, M KENWOOD |
| | HEINEMANN MODULAR MATHS FOR EDEEXCEL AS & A-LEVEL PURE MATHS -4 | GEOFF M, M KENWOOD |
| | HEINEMANN MODULAR MATHS FOR EDEEXCEL AS & A-LEVEL PURE MATH -5 | GEOFF M, M KENWOOD |
| | PURE MATHEMATICS (NEW EDITION) | BACKHOUSE |
| **GENERAL STUDIES** | DEMOCRACY AND DEVELOPMENT | BHANGWATI J, N 2002 |
| | THE CONCEPT AND THEORIES OF MODERN DEMOCRACY | BIRCH A.H 1993 |
| | COLLINS DICTIONARY OF ENVIRORNMENTAL SCIENCE | GOILLIER et al (1990) |
| | FOREIGN POLICY OF TANZANIA 1961-1981 | MATHEW, K &S. MUSHI |
| | TECHNOLOGY AND INDUSTRIALIZATION IN AFRICA ,DAKAR | YASHIR F. (1987) |
| **GEODGRAPHY** | LANDFORMS FOR AFRICA | COLIN BACON |
| | PRINCIPLES OF PHYSICAL GEOGRAPHY | MONKHOUSE |
| | PRACTICAL GEOGRAPHY | PRITCHARD |
| | PHYSICAL GEOGRAPHY | ZIST |
| | HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY | GOH |
| **ECONOMICS** | PRINCIPLES OF ECONOMIACS | JHINGAN M.L ) 3RD |
| | PRINCIPLES OF ECONOMICS | DWIVED D,N 3RD |
| | AN INTRODUCTION TO ECONOMIC THEORY | GUPTA ,B.L 3RD EDITION |

| | | |
|---|---|---|
| | MODERN ECONOMICS THEORY | K.K DEWETTA&M.H NAV |
| **CHEMISTRY** | ESSENTIALS OF PHYSICAL CHEMISTRY<br>ESSENTIALS OF ORGANIC CHEMISTRY<br>ESSENTIALS OF INORGANIC CHEMISTRY<br>CALCULATION FOR A-LEVEL CHEMISTRY<br>CONCEPTUL CHEMISTRY FOR CLASS XI<br>CONCEPTUL CHEMISTRY FOR CLASS XII<br>ENVIRONMENT AND SOIL CHEMISTRY | CHAND'S<br>CHAND'S<br>CHAND'S<br>E.N RAMSDEN 4TH ED<br>DR.S.K JAIN<br>DR.S.K JAIN<br>NGAIZA |
| **PHYSICS** | PRINCIPLES OF PHYSICS FOR XI<br>PRINCIPLES OF PHYSICS FOR XII<br>ADVANCED LEVEL PHYSICS | V.K MEHTA ,R MEHTA<br>V.K MEHTA ,RMEHTA<br>NELKON AND PARKER |
| **BIOLOGY** | NEW UNDERSTANDING BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL<br>BIOLOGICAL SCIENCE<br>BIOL0GY A FUNCTIONAL APROACH<br>BIOLOGY FOR CLASS XII AND XI<br>ADVANCED BIOLOGY ,<br>ELEMENTS OF BIOLOGY ,4TH ED 1997 | GLENN & S.TOOLE 4 ED<br>D.J TAYLOR ,N.O GREEN<br>M.B.V ROBERT<br>DR P.S, B.PPANDEY<br>R ,MREISS& G.MONGER<br>P. WEISZ ,R.N. KEOGH |
| **KISWAHILI** | NADHARIA YA FASIHI NA UHAKIKI<br>NADHARIA YA LUGHA KIDATO CHA V& VI NA ELIMU YA JUU<br>MISING YA SARUFI YA KISWAHILI<br>KITANGULIZI CHA TAFSIRI<br>KAMUSI YA KISWAHILI SANIFU<br>SARUFI FAFANUZI YA KISWAHILI | MASUKO C SALUHAYA<br>MASUKO C SALUHAYA<br>KARANJA .P , J. HABWE<br>NA MASUKO J.<br>HAMISA<br>WAIHIGA G |
| **ENGLISH LANGUAGE** | ADVANCED LEVEL ENGLISH LANGUAGE 1 FORM 5&6<br>ADVANCED LEVEL ENGLISH PRACTICAL APPROCH 2ND ED<br>ADVANCED ENGLISH LANGUAGE FORM 5&6 OXFORD<br>STYLISTICS & COMMUNICATION IN ENGLISH | S.G.N,J.E.KINUNDA<br>N. ASHELI<br><br>SIMWAMBA M.A |
| BAM | BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL | SEPTEMI I |

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
SHULE YA SEKONDARI MINAKI
**FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI** **MSS.K5. A**

**1.** Jina lako kamili…………………………………………………
**2.** Kidato ulichojiunga hapa shuleni……………………. mchepuo…………………
**3.** Jina la mzazi/mlezi…………………………………………….
Anuani yake…………………………. Simu ya Ofisini……………………………. simu ya mkononi……………………………….
Kazi yake…………………………………………….

**4.** Mahali ulipozaliwa
(i) Mkoa……………………… Wilaya ………………… Kata……………
(ii) Tarafa……………………… Kijiji cha …………………………..
(iii) Tarehe ya kuzaliwa ……………………
**5.** Mahali unapoishi sasa………………………………………
Anuani yako…………………………..
Namba za simu……………………………
**6.** Dini/dhehebu lako……………………….
**7.** Unaishi na Baba tu/mama tu/wazazi wote/mlezi…………………………….

**8.** 1. Jina la shule za msingi ulizosoma……………………………
(i) Shule ya msingi ya ………………………………Anuani………………………….
(ii) Shule ya msingi ya ………………………………Anuani…………………………..
2. Jina la shule za sekondari ulizosoma……………………………………………....
(a) Shule ya sekondari uliyoanzia……………………………Anuani…………………..
(b) Shule ya sekondari uliyomalizia…………………………Anuani…………………..

**9.** Michezo unayocheza
(a)………………………………….
(b) …………………………………

**10.** Vyama vya kujifunza ambavyo wewe unapenda kuwa mwanachama:
Scout, Fema, Wapinga Rushwa(PPCB), YUNA, Mali Hai, Ant Aids, School Magazine na Mazingira.
(a)……………………………………………..
(b)………………………………………………
(c)…………………………………………………
**11.** Je unao ulemavu wowote? (Ndiyo / Hapana)
Kama Ndiyo taja aina ya ulemavu……………………………………………………..

**N.B:** Mazingira ya shule si rafiki kwa watoto wenye ulemavu.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE
SHULE YA SEKONDARI MINAKI

**FOMU YA UTHIBITISHO** **MSS.K5. B**

Fomu hii ijazwe na mzazi au mlezi wa mwanafunzi katika sehemu zake na irudishwe shuleni ikiwa imeambatanishwa na picha ya mzazi/mlezi. Shule itatoa taarifa kwa mzazi / mlezi ambaye picha yake na maelezo yake yataonekana katika fomu hii.

Mimi……………………………………………mzazi/mlezi wa Mtoto wangu……………………………………nimeona, nimeelewa na nimekubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari ya Minaki. Nitampa mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na walimu wa shule ya Minaki katika kumlea vizuri mtoto wangu ili aweze kusoma na kuelewa na hatimaye aweze kufanya mitihani yote ya ndani shuleni na ya Taifa kwa mujibu wa ratiba.

Saini ya mzazi/mlezi………………….

Anuani ya mzazi/mlezi

………………………..

……………………………

Simu…………………………

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI:**

Mimi………………………………………… mzazi/mlezi wa mwanafunzi……………………………………………wa kidato cha tano.

Nakiri kwamba yaliyoandikwa hapo juu kwenye fomu zote mbili (MSS.K5. A na MSS.K5. B) ni sahihi.

Picha ya mzazi/ mlezi

Picha ya mwanafunzi

**SAINI YA MZAZI/ MLEZI.**

……………………………………

Tarehe…………………………….

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE
SHULE YA SEKONDARI MINAKI

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA** **MSS.K5.ME**
(Request for Medical Examination)

This form is to be completed by a Medical Officer.

**Name of pupil…**…………………………… **Age:** ……... **Sex:** …………

The above named has been examined in respect of:

**(a) STOOL ……………………………………………………………………**

**(b) URINE ...……………………………………………………………………**

**(c) CHEST ………………………………………………......................................**

**(d) BLOOD ……………………………………………………………………….**

**(e) EYES ………………………………………………………………………**

**(f) EARS ………………………………………………………………………**

**(g) HEART ……………………………………………………………………...**

**(h) STOMACH ULCERS ……………………………………………………...**

**(i) OTHERS ……………………………………………………………………….**

I am satisfied **/** not satisfied that the above named Student is physically and mentally fit to pursue further studies in Secondary School.

**………………………………** **………………**
**SIGNATURE (and official stamp)** **DATE**

**………………………** **……………….**
**DESIGNATION** **STATION**

**N.B.** Fomu hii itajazwa na Daktari wa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe atakapofika Shuleni (na sio hospitali nyingine). Mwanafunzi atakapofika shuleni atapewa utaratibu na atagharamia shilingi Elfu Tano (5,000/=)

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
# SHULE YA SEKONDARI MINAKI
# SHERIA NA KANUNI ZA SHULE MSS.K5.C

**UTANGULIZI**

Shule ya sekondari Minaki ni taasisi ya elimu ambapo wanakaa na kuishi walimu na familia zao, wafanyakazi wasio walimu na familia zao na wanafunzi. Pia katika eneo la jirani na shule wapo wengine wanaoishi ambao ni watumishi wa kanisa la Angalikana – waanzilishi wa shule, watumishi katika jamii. Pamoja na kanuni na sheria za nchi, kila mwanafunzi anatakiwa kufuata taratibu/sheria za shule/Wizara ya Elimu kama ifuatavyo;

**A. HESHIMA:**

Katika kutekeleza suala la heshima shuleni yafuatayo yanatakiwa yazingatiwe:

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuwaheshimu walimu au mtu yoyote aliemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya na isiyo ya heshima wakati wowote kati yake na mwanafunzi mwenzake, kwa walimu wake au kwa mwingine yoyote.

(iii) Kila mwanafunzi anatakiwa ashirikiane vizuri na kuwatii walimu wake na wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.

(iv) Kila mwanafunzi anatakiwa ashirikiane vizuri na wanafunzi wenzake katika kazi halali za shule. Pia kila mwanafunzi anatakiwa kuthamini kazi za aina zote zinazotolewa.

(v) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:

  (a) Kufuga kucha, ndevu,nywele zisizo safi na kusuka rasta

  (b) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama; nguo zinazobana mwili, singlend, fulana/ shati zilizokatwa na zilizochorwa chorwa. Pia kukunja mikono ya shati, fulana na suruali.

  (c) Kumkimbia mwalimu, mfanyakazi wa shule.

  (d) Kubishana na mwalimu na kutomtii atoapo maagizo halali.

  (e) Kutokutii kengele ya shule.

  (f) Kudharau na kukejeli walimu, Wafanyakazi wasio walimu na viranja (viongozi).

  (g) Kugombana na mwanafunzi mwenzako au na mtu yeyote

  (h) Kuhifadhi silaha kama nondo,kisu, bisibisi,kiberiti na vitu vingine vinavyotishia amani na usalama.

(vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kuitikia mara moja na kukimbia aliko anayewaita.

(vii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, court of arm, Wimbo wa taifa, nyimbo za Tazama Ramani, Tanzania nakupenda, Wimbo wa shule na fedha.

(viii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu darasa, ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, ukumbi wa chakula, jiko, mali yake binafsi na mali ya umma.

(ix) Kila mwanafunzi anatakiwa kujipanga katika mstari, kuwa mtulivu na kufuata maelekezo ya walimu na viongozi(viranja), wakati wa kupokea huduma kama; chakula n.k.

(x) Mwanafunzi anatakiwa kutotoa matusi kwa mtu yeyote pia kutofanya vitendo vyovyote na ishara zinazoashiria kumdhalilisha mtu au jinsia.

(xi) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu walimu na wafanyakazi wote bila kujali jinsia ,rangi ,tofauti za kisiasa , kidini na kitamaduni katika jamii.

**B. MAHUDHURIO:**

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi (masomo) vyote darasani bila kukosa kwa kadri ya ratiba ya shule.

(ii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuaria na kufanya mazoezi yote, majaribio yote, mitihani yote ya ndani/nje ya shule na ya kitaifa.

(iii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria kazi za mikono na kushiriki.

(iv) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba (mabweni), mikutano ya darasa, michezo n.k.

(v) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano na makongamano ya vyama vya masomo, mijadala na vyama vya huduma za kijamii vilivyopo shuleni

**C. MAANDALIO YA JIONI (EVENING PREPARATIONS):**

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya jioni (evening preparations) bila kukosa. Maandalio ya jioni yataanza saa 1:30 jioni na kumalizika saa 4:00 usiku kila siku kwa siku za Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi na Ijumaa . Siku za jumamosi na Jumapili maandalizi ya jioni ni ya hiari kwa mwanafunzi. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalizi mchana kwa siku za weekends na sikukuu za kitaifa (isipokuwa za dini) kuanzia saa 8:00 alasiri hadi saa 10:00 jioni.

**D. KUWAHI:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kujenga tabia ya kutunza na kuthamini muda wakati wote akiwa shuleni na hivyo kutimiza yafuatayo:

(i) Kila mwanafunzi kuamka mapema alfajiri, kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwili na kuoga maji.

(ii) Kushiriki mapema shughuli za usafi wa kila siku, k.m kufagia chumba, bweni, darasa, kiunga , kudeki vyoo n.k.

(iii) Kuwahi katika shughuli za shule kama vile mstarini, darasani, katika maandalio ya jioni, katika ukumbi wa chakula, usafi wa bweni, darasani viunga vya bweni na darasani, michezo, n.k.

(iv) Kila mwanafunzi anatakiwa awahi apatapo taarifa ya kuitwa na walimu wake/ viranja

(v) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi anaposikia wito wa dharura.

(vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni na kuripoti ofisi ya malezi kwa tarehe iliyopangwa kila likizo na sio baada ya tarehe ya kufunga shule.

(vii) Mwanafunzi akichelewa kuja Shule baada ya likizo kuisha kuanzia siku ya kwanza unatakiwa uje shule ukiwa na mzazi/mlezi na usipokuja na mzazi/mlezi ukifika shule utarudishwa nyumbani na barua ya wito kwa mzazi/mlezi.

**E. SARE YA SHULE:**

Wanafunzi wanatakiwa kufahamu ya kwamba sare ya shule ni fahari, ni kiunganishi chao, ni utambulisho wao, ni heshima yao katika jumuiya ya shule na jumuiya zote za nje ya shule. Sare ya shule inatakiwa ivaliwe kwa heshima, wakati wote wa:-

(a) Masomo darsani

(b) Mwanafunzi anapotoka nje ya shule kwa shughuli zake na za kishule.

(c) Baraza, Mikutano na sherehe za shule.

(d) Mwanafunzi anapokwenda hospitali.

(e) Mwanafunzi anapokwenda katika maandamano ya kishule.
(f) Mwanafunzi anaposafiri kuja shuleni au kwenda likizo
(g) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za michezo wakati wa michezo mbalimbali shuleni.
(h) Mwanafunzi huruhusiwi kuvaa nguo/ sare ambazo sio za kidato chake.

**F. UMEME: -**

Ni marufuku kuunganisha umeme (illegal connections) kwasababu yoyote ile katika majengo ya shule kama ofisi, darasani, bwenini, jikoni , katika ukumbi wa chakula ,n.k.

(a) Mwanafunzi atawajibika na ulipaji gharama zote zitakazotokana na "illegal connection".
(b) Ni lazima mwanafunzi atoe taarifa za "illegal connections", za watu walioshiriki na sehemu zilizopo bila kuchelewa.
(c) Viongozi wa mabweni watawajibika kukagua" illegal connections" kila wakati.
(d) Ni marufuku mwanafunzi kutoa au kuhamisha balbu mahali ilipowekwa.

**G. MITIHANI**

a) Mitihani ni kipimo cha uelewa wa mwanafunzi katika masomo yake anayosoma shuleni. Mwanafunzi anapimwa kwa maswali ya mtihani ili mwalimu na mtahiniwa aweze kufahamu ni kwa kiasi gani mwanafunzi ameyaelewa aliyofundishwa. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani ili aweze kufanya mitihani na kufaulu mitihani yote.

b) Mwanafunzi akipata daraja la tatu, nne au sifuri kwa mitihani miwili mfululizo mzazi/mlezi ataitwa Shuleni kuja kujadili taaluma ya mtoto wake na walimu.

c) Mwanafunzi asipofanya mtihani bila kutoa taarifa mzazi/mlezi atagharamia gharama za kutungiwa mtihani mwingine, pia mwanafunzi atapewa adhabu nyingine ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.

d) Unatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote kwa kadri ilivyoanishwa katika utaratibu na ratiba ya shule bila kukosa. Ni kosa kubwa Sana kutofanya majaribio na mitihani inayoandaliwa ndani nan je ya shule. Aidha adhabau ya kukosa kufanya mitihani ni kama ifuatavyo:-

1. Wito kwa mzazi / mlezi. 2. Viboko vinne(4) mstarini(paredi)
3. Kutafuta shule nyingine 4. Kugharamia mitihani uliyokosa

**Mwanafunzi hatakiwa kufanya yafuatayo:**

(i) Kuogopa mtihani na hivyo kutokufanya mtihani kwa visingizio
(ii) Kuiba na kuibia mtihani
(iii) Kuchagua masomo atakayofanya katika mtihani na kuacha kufanya mengine.
(iv) Udanganyifu wa aina nyingine katika mtihani.

## H. MAZINGIRA:

Mazingira ni kila kinachotuzukunga katika muktadha hasa utunzaji wa miti , maua nyasi na mipango endelevu ya kupanda miti na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika shule yetu:- Katika kutekeleza majukumu hapo juu na mengine yanayohusiana na mazingira katika shule yetu kila mwanafunzi: -

(i) Anatakiwa kushiriki katika kuyatunza kuyahifadhi na kuyaendeleza mazingira ya shule yetu

(ii) Kujielimisha kuhusu majukumu ya kuendeleleza mazingira ya shule kupitia wanamazingira, vitabu na walimu waliopo shuleni.

(iii) Kushiriki katika kupanda miti, maua na nyasi na kuvitunza vizuri kwa mbolea na maji kwa manufaa ya shule

(iv) Kila mwanafunzi anatakiwa kuyathamini mazingira ya shule kwa kutoyaharibu kwa namna yoyote ile na kwa sababu zozote zile .

(v) Kila mwanafunzi anatakiwa kutoa mawazo na taarifa za kuendeleza mazingira ya shule .

(vi) Mwanafunzi hatakiwa kutupa takataka ovyo katika mazingira , darasani (karatasi), jikoni (mabaki ya chakula) bwenini (mabaki ya chakula ).

(vii) Ni marufuku kujisadia haja ndogo au kubwa sehemu tofauti na ndani ya choo au kuoga sehemu tofauti na ndani ya bafu, mfano nje ya darasa, bwenini kwenye viunga, vichakani, n.k.

(viii). Ni marufuku kutiririsha maji machafu kutoka madarasani na mabwenini wakati wa usafi

(x).Mwanafunzi hatakiwi kuhifadhi ndani ya chumba / bweni vifaa vya plastic zikiwemo chupa za maji isipokuwa ndoo tu .

(xi). Kila mwanafunzi anatakiwa kula chakula katika bwalo la chakula tu sio sehemu nyingine ya shule.

(xii).Mwanafunzi ukipita eneo ilipo bendera yaTaifa (SMAT AREA) unatakiwa upite ukiwa unakimbia na sio kupita ukiwa unatembea taratibu.Endapo utapita muda ambao bendera ndio inashushwa au inapandishwa unatakiwa kusimama hadi zoezi hilo limalizike.

## I. USAFI: -

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia usafi wa mwili wake kwa kuoga kila mara na kuvaa nguo safi wakati wote.

(b) Kila mwanafunzi anawajibika kuweka mazingira safi ya ndani na nje ya darasa, bweni, ukumbi wa chakula kwa:-

(i.) Kushiriki vizuri katika kazi za usafi anapopangiwa

(ii.) Kutochafua maeneo hayo kwa njia yoyote ile

(c) Kila mwanafunzi anatakiwa kufua sare ya shule na nguo zake (shuka ,neti, n.k.) , kila mara.

(d) Kutakuwa na ukaguzi wa usafi binafsi kwa wanafunzi wote kila siku ya Jumatano (paredi) ambapo walimu wote wa Shule wanakuwepo kufanya ukaguzi wa usafi kwa kila mwanafunzi mmoja mmoja.

(e) Kutakuwa na ukaguzi wa usafi wa madarasa na mabweni kila siku za Jumatano mchana na Jumamosi asubuhi ambapo mwanafunzi anatakiwa kuwepo pembeni mwa kitanda chake.

**J. UKUMBI WA CHAKULA NA JIKO: -**

(i) Kila mwanafunzi lazima kufika jikoni au kwenye ukumbi wa chakula kwa muda ulipangwa na kufuata utaratibu uliopagwa wa kuhudumiwa chakula.

(ii) Kila mwanafunzi anatakiwa awe kimya na mtulivu anapoenda katika ukumbi wa chakula na jikoni

(iii) Kila mwanafunzi anatakiwa avae nadhifu anapoenda katika ukumbi wa chakula na jikoni, nguo za kulalia, ndala, marapa na viatu vilivyowazi haviruhusiwi kabisa katika ukumbi wa jiko.

(iv) Ni marufuku kuleta na kutumia vyombo vya plastic kwa huduma ya chakula.

(v) Lazima mwanafunzi kufika katika ukumbi wa chakula na jiko kwa huduma ya chakula

(vi) Ni marufuku mwanfunzi kupiga mswaki na kunawa miguu karibu na jiko au karibu na ukumbi wa chakula.

(vii) Ni marufuku kubishana na kugombana jikoni na ukumbini.

**K. (a) MABWENI**

(i) Kila mwanafunzi siku za usafi ni lazima ashiriki kikamilifu katika shughuli zote za usafi wa bweni lake na kuhakikisha amekaguliwa.

(ii) Kila mwanafunzi anatakiwa aweke malazi na matandiko katika hali ya usafi kwa kufua mara kwa mara blanketi, shuka, chandarua na foronya

(iii) Kila mwanafunzi anatakiwa atunze vifaa vya usafi vya Bweni

(iv) Kila bweni linatakiwa lishiriki kikamilifu katika mashindano ya usafi

(v) Ni lazima kila mwanafunzi asafishe chumba au sehemu anayolala bwenini kila siku

(vi) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki silaha na vifaa hatarishi bwenini kama nondo, panga nyundo, mkuki, upinde, visu, rungu, bunduki n.k.

(vii) Ni marufuku Kwa mwanafunzi kujihamisha bweni alilopangiwa kwenda bweni asilopangiwa bila kibali maalumu.

(viii) Ni marufuku Kwa mwanafunzi kumuhifadhi chumbani au bwenini kwake mwanafunzi wa bweni nyingine bila kibali maalumu cha shule.Aidha ni marufuku kulalia kitanda cha mwenzako.

(viii) Ni marufuku mwanafunzi kumkaribisha au kumuhifadhi mgeni yeyote chumbani au bwenini kwake, au kanisani au msikitini bila ruhusa ya Mkuu wa Shule.

(ix) Ni lazima kila mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika usafi wa ndani ya bweni lake na nje , mazingira yaliyozunguka bweni lake ambapo kutakuwa na ukaguzi wa kamati maalum ya usafi kila siku ya Jumatano na Jumamosi.

**L. MASIJALA YA KUHIFADHI KUMBUKUMBU ZA WANAFUNZI; -**

(a) Ni lazima mwanafunzi anapofika shuleni kwa mara ya kwanza kuhakikisha anawekwa katika kumbukumbu muhimu kwa kuandikishwa katika madaftari ya usajili, mabweni, madarasa n.k

(b) Ni lazima mwanafunzi ataje jina lake sahihi lililo katika kumbukumbu za vyeti vyake vya shule za awali

(c) Haitakiwi na hairuhusiwi mwanafunzi kuandikisha jina analofurahia kuitwa au jina analotumia kwa utani.

(d) Mwanafunzi lazima aripoti na kujiandikisha katika ofisi ya malezi anapofika shuleni kwa mara ya kwanza, aendapo likizo na kila arudipo kutoka likizo.

(e) Ni lazima mwanafunzi kujiandikisha uwepo wake katika mikusanyiko shuleni ikiwemo mstarini, darasani katika kila kipindi(somo), maandalio ya jioni na bwenini

(f) Ikiwa mwanafunzi hataweza kuhudhuria mkusanyiko wowote mfano; asubuhi mstarini darasani , shughuli za usafi bwenini na darasani kwa sababu za ugonjwa n.k lazima atoe taarifa rasmi yenye vithibitisho sahihi kwa Mkuu wa Shule.

(g) Ni lazima mwanafunzi aitwe jina na kuandikishwa jina lake kabla au baada ya kipindi (somo) na mwalimu wa somo

**M. MAWASILIANO:**

(i) Mawasiliano ni jambo muhimu sana kwa binadamu yeyote. Mawasiliano holela hayaleti ustawi wa kimaendeleo badala yake hubomoa.

(ii) Shule ina mpangilio na utaratibu wa mwanafunzi kuwasiliana na mzazi au mlezi au yeyote nje ya shule. Utaratibu huu hutolewa na kuelezwa kwa mwanafunzi mara anapo ripoti shuleni .

(iii) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu ya mkononi shuleni. Mwanafunzi atakaye kamatwa na simu atanyang’anywa na haitarudishwa, aidha atapewa adhabu kali ikiwemo ya kufukuzwa shule.

**N. WAGENI:**

(a) Mgeni yeyote wa mwanafunzi ni lazima kuripoti kwa mwalimu wa zamu au ofisi ya utawala wa shule kabla ya kukutana na mwanafunzi aliyetembelewa

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kumpokea mgeni yeyote katika mazingira ya shule bila walimu kuwa na taarifa.

(c) Mwanafunzi haruhusiwi kumpeleka mgeni yeyote darasani, bwenini au ofisini.

(d) Mwanafunzi haruhusiwi kumpokea mgeni jioni au usiku akitembelea shuleni.Muda wa mwisho wa mgeni kuwepo ndani ya Shule ni saa 12:00 jioni.

(e) Ni marufuku Kwa mwanafunzi wa shule nyingine kutembelea shuleni usiku kwa kisingizio chochote kile.

(f) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufika na kukaa au kuzurula ndani ya maeneo ya shule bila kibali cha shule.

**O. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Kuunganisha umeme isivyo halali katika majengo ya shule.
4. Matumizi ya madawa ya kulevya na ulevi
5. Uvutaji bangi/sigara
6. Makosa ya jinai.
7. Kupigana au kupiga
8. Kuaharibu kwa makusudi mali ya mwanafunzi au mfanyakazi au mali ya umma.
9. Kudharau Bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
10. Kuoa
11. Kusababisha mimba ndani ya jamii ya shule na nje ya shule.
12. Kutoa mimba/kushiriki katika kutoa mimba
13. Kumdharau kiongozi (kiranja) au kumpiga.
14. Kumdharau mwalimu au mfanyakazi asiye mwalimu, kumdhalilisha, kumtishia au kumpiga.
15. Kugoma, kuchochea migomo, kuongoza migomo, kuvuruga amani, usalama na utulivu wa shule na jumuiya zilizopo shuleni
16. Kumiliki simu Shuleni,
17. Kutoroka Shule, kulala nje ya Shule bila ruhusa na kutohudhuria vipindi.
18. Kukataa adhabu uliyoadhibiwa na mwalimu kwa makusudi
19. Kupiga kelele/kusumbua wanafunzi wanaojisomea au waliolala,

TAMKO LA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI:

Nakubaliana kufauta taratibu na sheria za shule kama zilivyoainishwa hapo juu.

**JINA MWANAFUNZI…………..…………….** **JINA LA MZAZI/MLEZI……..……………..**

**TAREHE ………………………………** **TAREHE …………………………………….**

**SAINI YA MWANAFUNZI……………………** **SAINI YA MZAZI/MLEZI………………….**